Uongozi – Siri
Na Larry Chkoreff

Version 1.2
Desemba 2010

Kimetafsiriwa na kuchapishwa na:
Cistern Materials Translation & Publishing Center, Nairobi, Kenya
Barua pepe: info@cisternmaterialscenter.com
www.cisternmaterialscenter.com

Uongozi – Siri Kimechapishwa na discipleship curriculum na international School of The Bible Marietta, GA USA
info@isob –bible.org – www.isob – bible.org

Haki ya kumiliki © 2010 na Larry Chkoreff Kimechapishwa na International School of the Bible,
Marietta, Georgia, U.S.A.

Kitabu hiki ni mali ya mwandishi. Kinaweza kuchapishwa tena, iwapo tu kitachapishwa chote, kwa ajili ya kukisambaza bure (bila malipo). Hairuhusiwi kukibadili au kukihariri kwa njia yoyote ile. Kikichapishwa tena ni lazima kiwe na tangazo la miliki.

Vifungu vyote vya Biblia vimetolewa kutoka The Holy Bible in Kiswahili Bi UV052 BST/BSK © 2003 published by Bible Society of Kenya and Tanzania.

## Uongozi-Siri

Rafiki yangu Bob weber, kiongozi mmoja wa wa kanisa letu Mount Paran North Church of God, Yule tena anajulikana ulimwengu kwa kuwa mwalimu wa uongozi –kwa huduma kubwa na shirika, alifunza mimi na mistari kadhaa ya hii mafundisho.Alinipa mimi yale mambo ya kawaida yeye hufunza.Ilhali, nataka kufanya hii kuwa wazi ya kwamba si kila kitu kwa hii kitabu hasa ni wazo lake, kama nilivyo chukuwa mistari ya maelezo yake na kubadili na kuongeza kulingana na jinsi nilivyo sikia Roho Mtakatifu akiongozi mimi.

Kabisa tena nimetiwa moyo na Dr.kirk walters, Pastor wa Mount Paran North church of God katika Marett Georgia, U.S.A.Dr.Walters ni mmoja wa wale viongozi nimeweza kuwa heshimu sana. Aliweza kuchangia kwa dhamana kuu kwa hii tolea.

Kuna tofauti kati ya kusimamia na kuongoza.Si viongozi wote wanaweza simamia au ni wasimamizi, hata si wasimamizi au maneja wote ni viongozi.Wasimamizi husimamia biashara ama huduma, lakini, hao huhakikisha , kweli wafanyi kazi wote wamefanya kazi na ya kwamba matarajio ya mefikiwa.

Mimi mwenyewe sio msimamizi, lakini Mungu ameniweka ndani ya uongozi.Hii ni dhihirisho ya jinsi. Shule ya ISOB inavyofanya kazi.ISOB ni huduma inasimamiwa kutoka kwa "mizizi"wale watu wako huko nje wale hutumia vitabu vyetu,huamua jinsi gani huduma itafanya kazi. Mara mingi hao kweli hunifunza mimi ile wanaoita kiongozi.Kiongozi mzuri yeye halalamishi wanao mfuata .Naamini ya kwamba kiongozi mzuri yeye hufuata Mungu, na kutembea na yeye na tena muda kwa muda yeye huangalia nyuma iliaweze kuona nani anatembea na yeye.Wafuasi wale hufuata kiongozi kwa kujitolea.

# SIRI

Unaweza kushangaa sana kwa kile ninachoita siri ya uongozi ni rahisi sana kwamba unaweza kupata ni ngumu kuamini.

Ikiwa wewe ni mwamini naya Yesu Kristo tena kiongozi Yule mkuu wa kihistoria Yesu Kristo , huishi ndani yako kupitia Roho Mtakatifu.Yeye hutamani kuishi maisha yake kupitia wewe.Hii inaitwa neema.Ikiwa anaishi ndani yako , sasa nguvu zote za kuwa kiongozi mkuu,ulimwengu hujawahi jua inaweza dhihirika kupitia utu wako wewe mwenyewe.

**Wagalatia2:20inasema,**

*20 "Nimesulibiwa pamoja na Kristo, wala si mimi tena ninayeishi bali Kristo ndiye aishiye ndani yangu. Uhai nilio nao sasa katika mwili, ninaishi kwa imani ya Mwana wa Mungu, aliyenipenda na kujitoa kwa ajili yangu*. "

Kuna mambo mawili huwa inazuia hizi nguvu za uongozi kudhihirika ndani yako kupitia wewe.

1. Kukosa imani, na kuamini ya ukweli kwamba yeye huishi ndani yako na angetaka.Kuishi maisha yako yake kupitia wewe.

2. Kukosa kuungana na kuruhusu.Yeye kuendesha maisha yako kwa yale si yake inaitwa "ya mwili".

**Kutolewa kutoka sura "KUKAA"katika kitabu cha Kufa au Kukua**

Inayofuata ni ukweli wa Neno ile inapaswa kuipaswa kuifikiri katika maisha yako.Ukweli huu ni mbegu nzuri, ile itazaa matunda mazuri ndani ya maisha yako.

Roho Mtakatifu kupitia Neno anaweza fanya wewe ulivyo ndani ya Kristo kuwa ukweli unapaswa kuchukuwa Neno kwa uhalisi na kuiamini kama toleo iliyohalarishwa,amakubaliwa.

Ulikuwa umepotea bila tumaini.

Ulikuwa mfu ndani ya dhambi.

Damu yake Yesu alimwaga pale msalabani ilitoa dhambi zako.Akachukuwa nafasi yako.

Wewe ulikuwa ndani ya Kristo'Wakati haya yote ilikuwa ikikuwa ikitendeka.

Ulikufa pamoja na Kristo.

Ulizikwa pamoja na Kristo.

Ulifufuka pamoja na Kristo.

Hii ni msimamo halali na Mungu siku ya leo na msingi wa mambo iliyo halali. Mradi tu , ulimwengu wa kiroho unahusika , eneo lako liko na Kristo katika mbingu.Wewe uko kwa kiti cha Mamlaka .Shetani na akili zako zitakwambia wewe eti kwamba.Hujakaa naye Kristo katika mbingu, lakini hayo ni uongo!Unafaa kujua kwamba Mungu amekaa na na wewe hata wakati ulikuwa mwenye dhambi.

***Wewe ni kiumbe kipya.*** "Kwa hiyo kama mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita, tazama, yamekuwa mapya" (2Wakorintho5:17).

***Wewe ni mwenye haki.***

***Utawala wa shetani juu yako umevunja.***

Mungu aliumba kila mmoja wetu na kipawa, apesheli, nasi kila mtu aliitwa kuwa kile ulimwengu huita kiongozi. Ihali, naamini kwamba Mungu hutamani kufanya maisha yake kupitia kila mmoja wetu kama kiongozi kwa mtindo wa aina Fulani ama ingine.Kwa wale wenu wamekuwa kwa eneo la uongozi wa aina Fulani ,ikiwa ni huduma biashara ama kama kiongozi wa familia , uko na uweza wa kusababisha eneo lako la utawala na uongozi wa nguvu sana unao julikana na mwanadamu ! Mwanadamu! Unaamini haya?

Ndio ____________

La ______________

Sina uhakika , niambie zaidi____________

Yatufuatayo ni mambo makuu 14 kwa maoni yangu viongozi wanapaswa kueneza.Sikusema eti hii ni kwamba ni mambo yote, lakini haya ni iliyo ya muhimu sana kwangu mimi.

1. **Kiongozi wa kiungu kweli ni huduma pengine ielezewe katika Bibilia kama mtumwa.**

**(2 Wakorintho 4:5-7) Bibilia iliyofafanuliwa inasema**,

*"Kwa maana hatujihubiri sisi wenyeweila tunamhubiri Yesu Kristo kuwa ni Bwana na sisi ni watumishi wenu kwa ajili ya Yesu. Kwa kuwa Mungu, Yeye aliyesema, ''Nuru na ing'ae gizani,'' ameifanya nuru Yake ing'ae mioyoni mwetu ili kutupatia nuru ya maarifa ya utukufu wa Mungu katika uso wa Kristo. Lakini tunayo hazina hii katika vyombo vya udongo, ili ijulikane wazi kwamba uwezo huu wa ajabu unatoka kwa Mungu wala si kwetu***.**

Rafiki wangu mzuri Scott Rickles alisema jambo kwangu ya kweli inayoambatana na hii wazo.Alisema ni lazima tutii kuenenda kutoa dhabibu amakujitoa kwa wengine. Toka kwa mema yako ndio upeane mema kwa wengine.Jambo la shukrani kwako wewe.

Maandiko iliyo hapo juu inasema .Kwamba Mungu ameangaza mwangaza ndani ya mioyo yetu. Yesu alifanya hivyo kwa kuacha iliyo bora kwake ilikutopeana sisi iliyo bora , na akajua hakuna vile tungeweza kulipa yeye kwa hiyo.Iihali,fahamu ya kwamba sasa juu tumeweza kupata huu mwanga, tumeagizwa "kupeana" huu mwanga kwa wengine kama watumishi wao ama watumwa wao .Mtumwa hufanya kazi bila kutarajia malipo. Yeye hufanya kile mwajiri mema hivyo ndio tunafaa tuwe kwa wengine.

***Kiongozi ni lazima awe mtumishi au mtumwa.***

**Mathew20:20-28 inasema,**

*20 " Kisha mama yao wana wa Zebedayo akamjia Yesu pamoja na wanawe, naye akiwa amepiga magoti mbele yake, akamwomba Yesu amfanyie upendeleo.*

*21 Yesu akamwuliza, "Unataka nini?'' Akajibu, "Tafadhali, wape wanangu hawa, mmoja aketi upande wako wa kuume na mwingine upande wako wa kushoto katika Ufalme wako.''*

*22 Yesu akawaambia, "Ninyi hamjui mnaloomba. Je,ninyi mnaweza kunywea kikombe nitakachonywea mimi?'' Wakajibu, "Tunaweza.''*

*23 Yesu akawaambia, "Kwa kweli kikombe changu mtakinywea, lakini kuketi upande wangu wa kuume au wa kushoto, si langu mimi kuwapa. Nafasi hizo ni za wale ambao kwa ajili yao zimeandaliwa na Baba yangu.''*

*24 Wale wanafunzi wengine kumi waliposikia haya, waliwakasirikia hao ndugu wawili.*

*25 Lakini Yesu akawaita wote pamoja na kuwaambia, "Mnafahamu kuwa watawala wa watu wasiomjua Mungu huwatawala kwa nguvu, nao wenye vyeo huonyesha mamlaka yao.*

*26 Isiwehivyo kwenu. Badala yake, ye yote anayetaka kuwa mkuu miongoni mwenu hana budi kuwa mtumishi wenu,*

*27 Naye anayetaka kuwa wa kwanza miongoni mwenu ni lazima awe mtumwa wenu,*

*28 Kama vile ambavyo Mwana wa Adamu hakuja ili kutumikiwa, bali kutumika na kuutoa uhai wake uwe fidia kwa ajili yawengi''*

***Tunatumikia Mungu kwa kutumikia wengine ( Rick Warren)***

*"Lakini sivyo kwenu. Badala yake ye yete anayetaka kuwa mkuu miongoni mwenu hana budi kuwa mtumishi wenu." Mariko 10:43*

*Ulimwengu huelezea ukuu njia ya uweza, vitu sifa njema na hata eneo unalo shikiria.Ikiwa unaweza ulizwa kutumikiwa na watu,umefika.Katika utamaduni wetu wa kutumika,na mafikira ya ama mtindo ya mimi "ni mimi kwanza"kutenda kama mtumishi haina umarufu.*

*Yesu, ilhali aliweza kuupima ukuu kwa kutumika, lakini si kwa cheo. Mungu yeye huona ukubwa wako kwa jinsi ya watu wengi umetumikia lakini si ni wangapi wanakutumikia.*

*Hii ni kinyume cha hisia za ulimwengu wa ukubwa,ya kwamba, tuna wakati mgumu wakuelewa hii na tena kuifanya.Wanafunzi walibishana kuhusu nani anafaa kile cheo cha ukubwa,na baada ya miaka 2,000,vingozi wa kikristo bado tu wana ng'ang''ania hizo cheo na ukubwa katika kanisa, dini na huduma.*

*Vitabu vingi vimeandikwa kuhusu uongozi lakini vidogo sana kuhusu utumishi. Kila mtu anataka kuongoza: hakuna mmoja anataka kutumika.Afadhali tuwe jumla kuliko ndani .Hata wakristo wanataka kuwa "viongozi –watumishi".Lakini sio tu watumishi lakini kuwa kama Yesu ni kuwa mtumishi. Hivyo ndivyo alijiita yeye mwenyewe.*

*Unapojua umbo lako (kipawa chako)ni muhimu sana kwa kutumikea Bwana,kuwa na moyo wa kutumika,hii ni kuu na ya muhimu kabisa kukumbuka, Mungu alikuumba kwa utumishi si kwa kibinafsi. Bila moyo wa utumishi utajaribiwa kutumia vibaya umbo lako la ufanisi.Tena utajaribiwa kuitumia kama sababu ili kuondokea kutatua shinda zingine.*

*Mara nyingi Mungu hujaribu mioyo yetu kwa kutuliza kutumika kwa njia zile hajatuumbia .Ukiona mtu akianguka kwa shimo Mungu anatarajia wewe umsaidie yeye atoke lakini si kusema "mimi sina kipawa cha huruma ama utumishi"Unaweza kuwa hujapewa kipawa kwa kazi Fulani, unaweza itwa kufanya ikiwa hakuna mtu akona hicho kipawa karibu.Huduma yako ya msingi ni lazima iwe kwa eneo la umbo lako ,lakini huduma yako ya upili ni pahali unahitajikana kwa sasa.Umbo lako linadhihirisha huduma yako, lakini roho yako ya utumishi inaonyeshana ukomavu wako.Hakuna kipawa ama talanta inahitajika baada ya kukutana na kuchukuwa takataka ama rundo la viti.Kila mtu anaweza kuwa mtumishi.Unawezaje jua uko na moyo wa mtumishi? (Mathayo 7-16)*

**Mathayo 24:45-46 inasema,**

*45 "Ni nani basi aliye mtumishi mwaminifu na mwenye busara ambaye bwana wake amemweka kusimamia watumishi wengine katika nyumba yake, ili awape chakula chao kwa wakati muafaka?*

*46 Heri mtumishi Yule ambaye bwana wake atakapokuja atamkuta akifanya hivyo. Amin, amin nawaambia."*

**Kiongozi ni lazima awe "hakuna"**

Napenda hii wazo lilielezwa na Reinhart Bonnke ya kwamba nilisikia hivi karibuni. Alisema kuhusu wakati ule kwanza Mungu alinena naye kama kijana eti atahubiri injili njema Afrika yote.Wakati alimwambia babake akamwambia Reinhart "la umesikia Mungu vibaya"Ukweli yeye akisema ya kwamba nduguye mkubwa atatumiwa na Mungu na ataridhi huduma ya familia.Baada ya yote,babake akamwambia, "ndugu yako ni mzuri na hupata alama mzuri shuleni"Mambo ingine yote ilifanyika katika maisha ya Reinhart ilisababisha yeye kuwa "hakuna"(o)alama ambayo haina maana.Na kama wengi wenu wanapojua Reinhart Bonnke amekuwa kwa wakati wa kihistoria ,muijiristi mkuu ulimwengu unapojua, na hasa katika Afrika. Tena, Bonnke huelezea kwamba Yesu ndiye nambari moja 1.Ikiwa mtu Yule ni ataweka moja mbele na zote zitakuwa kumi, 10.Tena vile tu, uko na sufuria nyingi zimeongezewa,ndio namba inavyoendelea kuwa kubwa,1,000000.

Kumbuka Yesu. aliomba usiku kucha na ndio akawachagua kumi na wawili"sufuri"kuwa watumishi na wanafunzi wake.Wewe umehitimu kama "sufuri"?Tena hakikisha nambari moja iko mbele yako!

**Muhtasari:**

**2. Kiongozi ni lazima awe na maono**.

Hata watu wadunia wanajua bila maono hakuna nidhamu, hakuna uwezekano wa kufaulu.Mungu ni Mungu wa maono.Tazama hata katika uumbaji(ama kuumba tena)kwa kitu chochote kama imeelezwa sura ya kwanza ,Mungu alifanya na maono.

**Mwanzo 1:2 inasema,**

*"Sasa Dunia ilikuwa haina umbo tena ilikuwa tupu, giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji, naye Roho wa Mungu alikuwa ametanda juu ya maji."*

Mstari ifuatayo katika Mwanzo 1:2 inaelezea chochote Mungu aliumba kwanza ,Mungu aliona giza tena Mungu akaona maona ya mwangaza, tena Mungu akanena.

***Mungu huita zile vitu hazipo kana kwambo zipo.***

**Warumi 4:17 inasema**,

*17 "*Kama ilivyoandikwa: ''Nimekufanya wewe kuwa baba wa mataifa mengi.'' Yeye ni baba yetu mbele za Mungu ambaye alimwamini, Mungu awapaye ahadi waliokufa na kuvitaja vilevitu ambavyo haviko kana kwamba vimekwisha kuwako."

Uchunguzi ulifanywa katika Yale University baina ya 1952 mpaka1972. Waliohitimu waliulizwa waseme maono yao.Kwa maisha yao na wito wao.Ni 3% ya wale waliohitimu walikuwa na maono na ndoto zilizo na msingi na wakaziandika.Baada ya miaka ishirini na mbili, iligunduliwa ya kuwa wale 3%walikuwa na utajiri mwingi kuliko unganisho la unganisho la 97%!

**Mithali 29:18 inasema,**

*18* **"***Mahali pasipo na maono, watu huangamia, bali ana heri mtu yule aishikaye sheria."*

Mungu aliumba mtu kwa mfano wake mwenyewe.Sisi tuliubwa tuishi kwa maono, ya baadaye.Bila maono,mwanadamu hatakuwa na na maishi iliyo na nidhamu.Yeye atazunguka katika

mito mingi,huduma nyinyi na upelelezi mwingi, lakini hakutakuwa na “kiongozi kwa hiyo meli”wakuonyesha njia.

Nimesikia wakisema “kutofurahia si kujua kile unataka na kufanya bidii kuipata”Kile tumejitoa sisi kukuwa kiko na nguvu kuliko yote ya jana”

***Ni nini nguvu za maono?***

Hata kwa ulimwengu wa kidunia, viongozi wanajua ni vizuri kuwa na maono, na wanahitaji maono.Viongozi washirika wazuri wanajua ni lazima waumbe maono kwa wafanyi kazi wao na wafuasi, wao Hata madhebahu,viongozi wao hujua hizi nguvu, na hao huzitumia.Kuna nguvu ndani ya mwanadamu , hata wasioamini wanaweza tenda makuu kupitia nguvu za ndoto na maono.Ilhali hii siyo yake Mungu ama kuanzilishwa na Mungu.Watu hutumia kanuni za nguvu za maono kwa tamaa zao za kibnafsi.

***Nguvu zake huwapa watoto wake maono kupitia Neno lake;***
**Samueli 3:1 inasema,**

***“****Taa ya Mungu ilikuwa haijazimika bado na Samweli alikuwa amelala hekaluni***a*** mwa BWANA, ambapo sanduku la Mungu lilikuwako.”*

Watu wa dunia hawana faida ya kufurahia nguvu zote za maono hupeanwa na Mungu.Tofauti baina ya maono yake Mungu na maono ya mtu kujitafutia maono yake ni Neno lake ni mbegu iliyo hai nai itaweza kufanya maono kukamilika katika upatano na ushirikiano wa nguvu za mwanadamu .Si kwa nguvu zetu ya kwamba tunaimarisha maono yetu;lakini Neno lake.Kwa njia nyingine, sisi tukiwa na upatano na Mungu ,tunahitaji kusikia na kutii kile anasema kuhusu tunapondelea. Mungu amenipa maono kuandika kupitia Zaburi 68:11ile inasema, **“**Bwana alitangaza neno, kundi la wanawake likatangaza amri hiyo.

Mimi nimeitwa kuisikiliza sauti yake, kufanya kwa bidii kwa kuandika kutumia nidhamu nyamaza na kuchukuwa kamputa na

kuandika.Nimeitwa kusoma tena , na kuwapa wengine wasome tena na kufanya bidii Ilhali,si mimi hutangaza ile nimeweza kuandika kwa rundo ya nchi.Si mimi hufanya wanafunzi.Neno lake hufanya hiyo yote. Neno lake ni mbegu.Neno lake lina nguvu zizizo za kawaida**.**

***Yeye hupee nani maono?***

***Waume na wake walio na "mioyo mwema"***

**Luke 8:15 inasema,**

*15 " Lakini habari zake Yesu zikazidi sana kuenea kotekote kuliko wakati mwingine wowote, makutano makubwa ya watu yalikuwa yakikusanyika ili kumsikiliza na kuponywa magonjwa yao."*

***"Watu walisaa limoja"wanaweza kumsikia MUngu vizuri na kwa hivyo kupokea maono yake.***

**Mathayo 20:6-8 inasema**,

*'' 6 Mnamo saa kumi na moja akatoka tena akawakuta wengine bado wamesimama bila kazi. Akawauliza, 'Kwa nini mmesimama hapa kutwa nzima pasipo kufanya kazi?'*

*7 Wakamjibu, 'Ni kwa sababu hakuna yeyote aliyetuajiri.' Akawaambia, 'Ninyi nanyi nendeni mkafanye kazi katika shamba langu la mizabibu.'*

*8 "Ilipofika jioni, yule mwenye shamba la mizabibu akamwambia msimamizi,'Waite hao vibarua na uwalipe ujira wao, ukianzia na wale walioajiriwa mwisho na kuishia na wale walioajiriwa kwanza."*

***Unaweza kuwa umeitwa kuunganisha katika maono ya mtu mwingine.***

Kuwa mwangalifu kukuwa na hisia na usidharao hii.Kawaida ikiwa Mungu amekuita kuungana na maono ya mwingine, wewe utajipata ama utagundua maono ile Mungu amekupa wewe itaungana naye huyo mwingine na mwili wa Kristo utajirike.

**Muhutasari:**

**3. Elezea maono yako kwa wengine.**

Nena Neno kwa nguvu. Daudi aliongea na Goliatho.Kunena ni muhuri wa kujitoa kwa maono.Maneno yalionenwa ni nguvu za kiroho.

**Warumi10:9-10 inasema,**

*9 "Kwa sababu kama ukikiri kwa kinywa chako kwamba ''Yesu ni Bwana.'' na kuamini moyoni mwako kwamba Mungu alimfufua kutoka kwa wafu, utaokoka.*

*10 Kwa maana kwa moyo mtu huamini na hivyo kuhesabiwa haki, tena kwa kinywa mtu hukiri na hivyo kupata wokovu."*

Haya yakisemwa, kuwa na uhakika ya kwamba utachukuwa na kuchagua ni nani utaelezea maono yako.Watu wengine watajaribu kukuvunja moyo na kukupa shuku.Wengine wata kutia moyo na kukuweka nguvu imani yako."

**Muhutasari:**

**4. Chunguza chochote.Uaminifu unahitajika.**

***Kutambua:***

Kuwa mwangalifu kuchunguza mambo yote kwa Roho Mtakatifu.Uliza yeye, atambue ukweli kuhusu ile jambo na hasa kuhusu watu. Watu wengine wanaweza kundanganya hata sisi. Lakini tunaweza tegemea Roho Mtakatifu atuonyeshe ukweli.

**Mithali 2:3-8 inasema,**

*3 **“**na kama ukiita busara na kuita kwa sauti ufahamu,*

*4 na kama utaitafuta kama fedha na kuitafuta sana kama hazina iliyofichwa,*

*5 ndipo utakapoelewa kumcha BWANA na kupata maarifa ya Mungu.*

*6 Kwa maana BWANA hutoa hekima, na kinywani mwake hutoka maarifa na ufahamu.*

*7 Huifadhi ushindi kwa ajili ya mwadilifu, yeye ni ngao kwa wale wasio na lawama,*

*8 kwa kuwa hulinda mwenendo wa mwenye haki na kuhifadhi njia ya waaminifu wake.”*

***Uaminifu wako wewe mwenyewe:***

Mungu alifanya kazi pekee kwa Uaminifu! Kila uongo ama kutokuwa na ukweli inapatia shetani nafasi kufanya kazi .Ni mwanya tu umeutengeneza iliashike na afinyilie maisha yako.Mtu mmoja akasema “hakuna kipofu zaidi kama mtu Yule hataki kuona ukweli”

**Zaburi 51:6 inasema**,

*6 “Hakika Wewe wapendezwa na kweli itokayo moyoni, ndani sana ya moyo wangu wanifundisha hekima.”*

**Zaburi 85:10-11inasema,**

*10 “Upendo na uaminifu hukutana pamoja,haki na amani hubusiana.*

*11 Uaminifu huchipua kutoka katika nchi, haki hutazama chini kutoka mbinguni."*

**1 Yohana 1:7 inasema**,

**"***Lakini tikienenda nuruni, kama Yeye alivyo nuruni, twashirikiana sisi kwa sisi na damu yake Yesu, Mwana Wake yatusafisha dhambi yote."*

***Hifadhi Neno lako.***

Sababu ina tunaweza kumwamini Mungu na NENO Lake ni kwamba yeye handanganyi.Yeye hawezi kusema uongo.Waamini wengi hawaelewi moyo wake Mungu wakati wa "kukiri uchungu wake"

**Ifuatayo ni dondoo kutoka kwa Dr.Kirk Walters, Administrative Pastor for Mount Paran North Church of God in Marritta,Georgia U.S.A. Dr.Walters ni mmoja wa marafiki wangu na mchungaji.**

*Jambo moja la muhimu kuhusu uaminifu kwa kiongozi ni kama tunaongoza kwa motisha ama kwa kufinyiliwa imeelezewa na Webster Dictionary "kutawala ama kusimamia kwa nguvu ama vibaya kwa mapato ya kibnafsi.Motisha ni kupeana kama mkristo kiongozi,uaminifu wangu ni lazima uanze na sababu kuu kwa nini nafanya jambo.*

*Nataka kuongoza kanisa ndio wengine wanione kuwa mtumishi mkuu? Ikiwa jibu langu ni ndio (nikiwa kabisa mwaminifu kwangu) tena kuna uwezekano wa kufinyilia wengine ndio nikaweza kufikia lengo langu kuu nionekane nimefaulu.*

*Yesu akasema kwamba kuna watu watakuja kwake siku ya mwisho na kusema "mbinguni. "Wengi wataniambia siku ile, 'Bwana, Bwana, hatukutoa unabii kwa jina lako na kwa jina lako kutoa pepo na kufanya miujiza mingi? Ndipo nitakapowaambia wazi,``Sikuwajua kamwe. Ondokeni kwangu, ninyi watenda maovu!' (Mathayo7:22-23). Yesu anasema hatuwezi kutumia jina lake ukuu*

*wake kuimarisha mapenzi yetu.Anasema ya kwamba "Si kila mtu aniambiaye, 'Bwana, Bwana,' atakayeingia katika Ufalme wa Mbinguni bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni"( Mathayo 7;21) ndio watakubalika kwa ufalme wake lakini ikiwa nia yetu ni kuongoza watu kwa mapenzi yake Mungu kamili ,kwa kuachilia neno lake kupitia mahubiri, mafundisho na uongozi wa utumishi ,nia zetu ziko safi na Mungu hakika atabariki jukumu letu.Ukweli kuna sababu tatu watu watafuata wengine:*

*1. Maono - Maono hushika mawazo ya mtu anapiga picha kwa akili vile siku sijazo zitakuwa.*

*2. Upendo - Upendo hushika moyo wa mtu, kwa kupiga picha ya jinsi watu wana kuwa.*

*3.Tabia - Tabia huleta mabadiliko.Watu hufuata mtu aliye na tabia,hata kama kabisa hawajaelewa maono yake.Wakati tunapewa motisha na maono matakatifu,upendo wa kiungu na tabia ya kikristo, watu watavutia nayo na kuamulishwa kufuata sisi.Watu kila mara hutazamia mtu wa kufuata.*

*Uongozi huanza na kiwango cha ukamilifu, kuhusu nia zetu.Wakati kiongozi mara kwa mara hutahini nia zao, wengine, pengine kuwa na swali ya tabia ya kiongozi na umarufu wake.*

***Kujitoa kwa Watchman Nee.***

*"Kuhusu matendo ya wanadamu, kwa neno la midomo yako, nimejiepusha na njia za jeuri." Zaburi 15:4.*

*Katika hali ile ya kukubaliana, neno la Wakristo limepewana, walio na ahadi lazima waheshimiwe.Kwa sababu Mungu alihifadhi neno lake la wokovu; yeye ni mwamini kwa ahadi zake. Gibeoni walindanya Joshua, na wakakubaliana wawe na hali ya amani kati yao kabla hawajagundua mipango yao. (Joshua 9:19)Hata kama Mungu alisisitiza kwamba neno agano kuheshimiwa na nyumaye kufungia mvua kwa sababu mfalme Sauli alienda kinyume na hiyo.*

*Mungu hakukubali sisi kuweza kuharibu agano kwa madharao.Yeye aliweza kufanya watu wa Gibeoni wahifadhiwe na*

*nyumaye akaamuru mfalme Daudi awalipishie, kwa uovu uliotendwa kwao, tarajia sisi tuwe kweli kwa maneno yetu,hata kama kwetu sisi tutaumia.*

**Muhutasari:**

**5. Badilisha mambo yasiyohitajika maishani mwako.**

Kuwa na nidhamu ya kuelekezea mambo muhimu na kuondoa isiyo na maana.Kuwa mwangalifu si kutatua kila shinda ile huja kwa njia zako.Yesu hakushughulikia kila hitaji lilikuja kwa njia zake.Mara nyingi alitumia wakati wake kwa kuomba na kukesha ,na baba Yule aliongoza na kumpa mwelekeo wa mambo yote yake .Alijua hivi wakati wa maombi yake vile Baba alitaka yeye afanye.

**Yohana 5:19 inasema,**

*19 "Yesu akawaambia, Amin, amin nawaambia, Mwana hawezi kufanya jambo lo lote peke yake, Yeye aweza tu kufanya lile analomwona Baba yake akifanya, kwa maana lolote afanyalo Baba, Mwana pia hufanya hivyo hivyo."*

**Yohana 12:20-26 inasema,**

*20 " Basi palikuwapo Wayunani Fulani miongoni mwa wale waliokuwa wamekwenda kuabudu wakati wa Sikukuu.*

*21 Hawa wakamjia Filipo, ambaye alikuwa mwenyeji wa Bethsaida huko Galilaya, wakiwa na ombi, wakamwambia, Tungependa kumwona Yesu.''*

*22 Filipo akaenda akamweleza Andrea, nao wote wawili wakamwambia Yesu.*

*23 Yesu akawajibu, "Saa imewadia ya Mwana wa Adamu kutukuzwa.*

*24 Amin, amin, nawaambia, mbegu ya ngano isipoanguka ardhini na kufa, hubakia kama mbegu peke yake. Lakini ikifa huzaa mbegu nyingi.*

*25 Mtu yeyote anayependa maisha yake atayapoteza, naye ayachukiaye maisha yake katika ulimwengu huu atayaokoa hata uzima wamilele.*

*26 Mtu ye yote akinitumikia lazima anifuate, nami mahali nilipo ndipo mtumishi wangu atakapokuwa. Mtu akinitumikia, Baba Yangu atamheshimu."*

**Muhutasari:**

**6. Jihusishe na washindi.Toka kwa wale hufikiria kinyume.**

Kaa karibu na Yesu.Chagua rafiki yako.Chagua rafiki unayetaka kufanana naye.Andika yale ungeyataka. Iwe ni ujuzi ama nia?Wewe uko na mamlaka juu ya nia zako .Chagua Yule ungetaka kuwa na kufanana naye.Andika sifa zao.Tena fanya uchunguzi kama sifa zao ni ujuzi ama nia.Wewe una 100%utawala wa hisia zako.Kweli mifano yetu kuu ni kujifananisha naye Yesu.Kuendelea kumjua yeye vizuri,naye atafanya kuiga ndani yako kwa neema yake.

**Muhutasari:**

**7. Fanya mazoezi ya bidii yako.**

Anza na kipawa kimoja kama Mathayo 25 wengi hupenda kuanza na vipawa tano au kumi:Mungu atafanya uhitimu kama utatumia kile kiko mikononi mwako,kama unafanyia Mungu na nguvu zako zote ,kile mikono yako itapata kukifanya.Hakuna msongamano wa kuenda hatua ingine mbele.

**Mithali 21:5 inasema,**

*5 "Mipango ya mwenye bidii huelekeza kwenye faida,kama vile kwa hakika pupa huelekeza kwenye umaskini."*

Weka bidii katika uhusiano si kwa mkono wa kazi.Kuna mapato ya upendo.Watu wengine wanasema "Siwezi ni kawa mkuu mpaka niwe na huduma na biashara yangu"Ile sehemu haija nenwa ya huo mstari kwa muda, ama sasa hivi sitajitoa kwa hii kazi ama hii huduma mpaka nipate yangu"Mungu hatabariki hiyo nia.

***Kuingia kwa sabato ya Mungu.***

Wakati tulipoitwa kufanya kazi kwa kijitoa kwa vitu tulizo nazo mikononi,sisi tumeitwa tena kuingia kwa pumziko lake,Waebrania sura ya 3 na 4.Hii inakaa kama fumbo lakini kweli siyo .Mungu anataka kubadilisha sisi kutoka "wakulima wa mimea"na kuwa watu wa kuzaa matunda. Mkulima wa mimea yeye hulima kwa shamba ,ngano mahindi na vingineo.Ni lazima apande kila mwaka na aruhusu pumziko (mzunguko)baada ya miaka saba. Mzalishaji matunda yeye hushughulikia matunda bado akiangalia nguvu za mbegu za kiungu ile ina ongezeka kila mwaka, ikitoa ama

kuzaa zabibu ama matunda mengine.Kwa mfano zaidi ya kufikiria kwake. Yesu akasema.

**Yohana 12:24inasema,**

*24 "Amin, amin, nawaambia, mbegu ya ngano isipoanguka ardhini na kufa, hubakia kama mbegu peke yake. Lakini ikifa huzaa mbegu nyingi."*

**Marko 4:8 inasema,**

*8 "Mbegu nyingine zilianguka kwenye udongo mzuri, zikaota vizuri na kukua, zikatoa mazao, moja thelathini, nyingine sitini na nyingine mia moja."*

**Dondoo kutoka kwa Watchman Nee:**

*Toshereko la kumanisha kwa sabato huja kwa kuingia katika pumziko lake Mungu.Ihali kuingia kwa pumziko lake Mungu, ni lazima tukubali kazi yake.*

*Hapa, tena ni sheria ya kukuongoza kwa maisha yetu yote ya kiroho.Ni lazima tuingie kwa pumziko letu. Kabla ya tuwe sehemu ya kazi yake. Ila baada ya kuingia katika pumziko tumehitimu machoni mwake Bwana, kuinuka na kumtumikia. Nani wale tu husikia na kulishika Neno lake huingia. Katika pumziko, lakini si kwa kazi!*

**Muhutasari:**

**8. Pita matarajio ya kawaida.Ruhusu Mungu akafanye kazi zaidi ya uwezo wako. Tafuta njia zote:**

Kwanza, utajaribiwa kutarajia tu Mungu akafaNye kile unaweza kufanya.Hii ni kwa sababu Mungu si wa haraka .Anaweza kuwa akichelewesha mambo mpaka tabia yako iwe sawa na yake ,na mpaka wakati wake ule unafika.Lakini inapokuja ;wewe kujichunga!Kama nilivyo taja hapo juu ,matunda kutoka kwa Mungu niya kiungu.Hukua kama kipepeo husisho.Ruhusu Mungu akuwezeshe kufikiria. Kutoka nje ya saduku, na uruhusu Mungu "nje ya saduku"awaze kuongea nawe.Dhubutu kuwa tofauti, wakati unaongozwa na Mungu .Mara nyingi Mungu hufanya mambo kinyume na matarajio yake mtu. Ikiwa unataka lazima upeane na kadhalika.

Ruhusu Mungu akupeleleze njia mpya na tofauti.Mara nyingi, hasa wakati ule mwingi, Mipango yake Mungu kabisa huwa tofauti na yangu.Ruhusu Mungu kabisa afanye jambo,ile kinyume na hujawahi jua hapo mbeleni kuwa mwenye hisia kwa hali kwa mawazo ya watu wengine, na kwa hiyo sauti iliyo ndani yako

**Waefeso 3:20 inasema,**

*20 "Basi kwa Yeye awezaye kutenda mambo ya ajabu yasiyopimika kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya uweza Wake ule utendao kazi ndani yetu."*

**Yohana 6:9-13 inasema,**

*9 "Hapa kuna mvulana mmoja mwenye mikate mitano ya shayiri na samaki wawili wadogo. Lakini hivi vitatosha nini kwa umati wote huu?''*

*10 Yesu akasema, "Waketisheni watu chini.'' Palikuwa na majani mengi katika eneo lile, nao watu wakaketi, palikuwa na wanaume 5,000.*

*11 Ndipo Yesu akachukua ile mikate, akamshukuru Mungu na kuwagawia wale watu waliokuwa wamekaa kwa kiasi walichohitaji.*

*Akafanya vivyo hivyo na wale samaki. Kila mtu akapata kadri alivyotaka.*

*12 Watu wote walipokwisha kula na kushiba, akawaambia wanafunzi wake, "Kusanyeni vipande vilivyobaki vya ile mikate, kisipotee cho chote.''*

*13 Hivyo wakavikusanya wakajaza vikapu kumi na viwili kwa vipande vilivyobaki vya ile mikate mitano na samaki wale wawili wadogo.*

**Muhutasari:**

9. **Kiongozi ni lazima awe chini ya mamlaka, ama yeye hatakuwa na mamlaka ya kiungu.**

***Mara nyingi Yesu huchagua watu wakamwakilishe kwa mamlaka yake.***

Hii inaweza kuwa kiongozi wa biashara yetu, Waajiriwa,wahubiri, na hata mamlaka ya kiserikali.Ni lazima tutii sheria za pahali na utawala tuliyo pewa, ikiwa hizo sheria hazija kiuka Neno la Mungu. Petro akasema vizuri. "Petro na wale mitume wengine wakajibu, Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu" (Matendo 5:29).

***Kuna kanuni ya mamlaka katika Mathayo 20.***

Kunalo jambo la uongo kwa kuwa chini ya unyenyekevu inamaanisha kuwa mnyonge.

Mamlaka ni nini? Inakuwa haieleweki.Dunia husema kwamba mamlaka ni kuongoza mtu.Yesu alisema mamlaka ni kuwa na mtu aliyeajika kwake.Kumshughulikia.

**Mathayo 20:25-28 inasema,**

*25 Lakini Yesu akawaita wote pamoja na kuwaambia,"Mnafahamu kuwa watawala wa watu wasiomjua Mungu huwatawala kwa nguvu, nao wenye vyeo huonyesha mamlaka yao.*

*26 Isiwe hivyo kwenu. Badala yake, ye yote anayetaka kuwa mkuu miongoni mwenu hana budi kuwa mtumishi wenu,*

*27 Naye anayetaka kuwa wa kwanza miongoni mwenu ni lazima awe mtumwa wenu,*

*28 kama vile ambavyo Mwana wa Adamu hakuja ili kutumikiwa, bali kutumika na kuutoa uhai wake uwe fidia kwa ajili ya wengi.''*

***Sheria ya mamlaka:*** Kama sheria za mvutano ama kuinua ni sheria ya kawaida, ama kama sheria ya maisha ya Roho katika Kristo Yesu ni sheria ya kiroho , kuna sheria ya kiroho, ni lazima ikafanye kazi na mamlaka.Kwa kifupi huenda hivi:Yule ananyenyekea kwa mamlaka atapokea Baraka zake na laana zake .Hii ni mpaka, huduma, tegemea ama kukosa hutegemea ni nani hasa umenyenyekea kwake .Kuingiza ndani ya hii ni eti mfano wa mamlaka.Hawaiwezi kushughulikia mtu,ikiwa yeye hajanyenyekea mfano mamlaka ukweli utaharibika.Mimi niko na hali niliyoshuhudia kwa upande mbili na ninaweza shuhudia hii sheria hufanya kazi.

***Katika Mathayo 8 Centuriani alikuwa chini ya mamlaka.***

Kwa nini Yesu akawa amefurahishwa naye hivyo.Katika Mathayo 8 wakati alisema atapona. "Lakini yule jemadari

akamwambia, “Bwana, mimi sistahili Wewe uingie chini ya dari yangu. lakini sema neno tu, naye mtumishi wangu atapona.Kwa kuwa mimi nami niko chini ya mamlaka, nikiwa na askari chini yangu. Nikimwambia huyu ‘Nenda,’ naye huenda, na mwingine nikimwambia, ‘Njoo’, huja. Nami nikimwambia mtumishi wangu, ‘Fanya hivi,’ hufanya’’ (Mathayo 8:8-9). Neno husema kwamba.Yesu alishangaa na kuwaambia wanafunzi wake kwamba hajaona imani iliyo kubwa kiasi hicho,hata kwa watu wa wanafunzi wake kwamba hajaona imani iliyo kubwa kiasi hicho, hata kwa watu wa agano Israeli Yule akida aliponywa hiyo saa. Imani na mamlaka iko na nini sawa?Ziko na uhusiano .Imani haiwezi kuwa bila mamlaka Imani bila matendo imekufa.

***Hawa watu walibarikiwa kwa kutii mamlaka.***

2 Wafalme 5:1 -Uponyaji wa mkuu wa Syria .Mkuu wa Kisyria akajaribu kutumia mamlaka juu ya Elisha ili mahitaji yake ikashughulikiwe (2 Wafalme 4). Alitaka kuwa mkubwa na kuita mlio. Lakini vile tu aliweza kunyenyekea kwa mamlaka akaponywa. Kutokana na ugonjwa wa ukoma.

Katika 1wafalme 17:9 yule mama mjane alinyenyekea kwa Elia, na badala ya kufa na njaa wawili walilishwa kwa njia ya kiungu kwa mwaka mzima.Nyumaye wakati mtoto wake alikufa aliweza kufufuka.Akapata Baraka kwa kutii.

Mimi nimeweza kubarikiwa juu ya kiwango katika ulimwengu wa biashara kwa “kuhitimu shule ya Mungu ya mamlaka baada ya miaka minane.Sijaelewa kama mtoto anayeelewa mamlaka.Kwa hivyo nilivyo kutana naye Yesu, akanionyesha kukaa katika mamlaka”Naweza kusema hivi kujitahidi kutii kwa mamlaka ya kuchaguliwa italeta Baraka zile hakuna mwanadamu anaweza kuzalisha!

***Wakati tunapotii Mungu tunapokea Mamlaka.***

Katika fumbo iliyo mathayo 19,tajiri alikuja nyumaye kuona kama walikuwa watiifu.Aliwapa,wale wahuduma,mamlaka mengi.

**Muhutasari:**

**10. Kiongozi ni lazima afanye kazi katika ufalme wa Mungu kwa eneo la kifedha.**

**Mathayo 6:33inasema,**

*33 "Lakini utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu na haki yake na haya yote mtaongezewa."*

***Kulipa fungu:***

Niliposoma kwa undani maandiko kuhusu kulipa fungu,la kumi kwa ongezeko lako kwa Mungu, ni gundua hatimaye rahisi sana.Huo ndio ulimwengu wa fedha chini ya laana, kwa sababu iko na mkuu wa ulimwengu shetani.

Ilhali ukishatoa fungu la kumi unaosha zile 90%zimebakina maisha yako ya kifedha haiku chini ya utawala wa kishetani.

**Malaki 3:10 inasema,**

*10 " Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu. Nijaribuni katika hili,'' asema BWANA Mwenye Nguvu, ''nanyi mwone kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni na kuwamwagieni baraka nyingi mpaka mkose nafasi ya kutosha au la."*

Maoni yangu kuhusu dirisha za mbinguni ni kwamba tunafaa,tusitarajie pesa kutoka mbinguni zianguke,lakini neno la kipekee lake mbegu.Wakati mbegu lake huanguka katika mioyo yetu, tena Baraka zitakuja.

**Mithali 3:9-10 inasema,**

*9 "Mheshimu BWANA kwa mali zako na kwa malimbuko ya mazao yako yote,*

*10 ndipo ghala zako zitakapojaa hadi kufurika, viriba vyako vitafurika kwa mvinyo mpya."*

***Kutoa***

Luke 6:38 inasema,.

*38 "Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa. Kipimo cha kujaa na kushindiliwa na kusukwasukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile kile mpimacho, ndicho mtakachopimiwa."*

Sheria ya kupeana si tu kwa pesa, hata huenda kwa kila chochote kiko kwa kipawa chako cha kupeana.

***Nondo na kutu***

**Mathayo 6:19-21 inasema,**

*19 "Msijiwekee hazina duniani, mahali ambapo nondo na kutu huharibu, nao wevi huvunja na kuiba.*

*20 Lakini jiwekeeni hazina mbinguni, mahali ambapo nondo na kutu haviharibu, wala wevi hawavunji na kuiba.*

*21 Kwa sababu mahali akiba yako ilipo, hapo ndipo pia moyo wako utakapokuwa.''*

***Mavuno mengi, tamaa***

**Luke12:15-34 inasema,**

*15 "Ndipo Yesu akawaambia, "Jihadharini! Jilindeni na aina zote za choyo. Kwa maana maisha ya mtuhayatokani na wingi wa mali alizo nazo."*

*16 Kisha akawaambia mfano huu: "Shamba la mtu mmoja tajiri lilizaa sana.*

*17 Akawaza moyoni mwake, 'Nifanye nini? Sina mahali pa kuhifadhi mavuno yangu.'*

*18 “Ndipo huyo tajiri akasema, ‘Nitafanya hivi: Nitabomoa ghala zangu za nafaka na kujenga nyingine kubwa zaidi na huko nitayahifadhi mavuno yangu yote na vitu vyangu.*

*19 Nami nitaiambia nafsi yangu, ‘Nafsi, unavyo vitu vingi vizuri ulivyojiwekea miaka mingi. Pumzika, ule, unywe, ufurahi.’ ’’*

*20 “Lakini Mungu akamwambia, ‘Mpumbavu wewe! Usiku huu huu uhai wako unatakiwa. Sasa hivyo vitu ulivyojiwekea akiba vitakuwa vya nani?’*

**Chagua vile unataka kuona maisha yako yakifedha.**
**Mifuko , pipa, kikapu ama ghala.**
**Mifuko iliyo na mashimo.**

**Hagai 1:6 inasema,**

*6 “Mmepanda vingi, lakini mmevuna haba. Mnakula lakini hamshibi, mnakunywa, lakini hamtosheki. Mnavaa nguo, lakini hamsikii joto. Mnapata mishahara, lakini inatoweka kama imewekwa kwenye mfuko uliotoboka toboka.’’*

***Pipa kulisha familia yako.***

**2Wafalme 4:1-7 inasema,**

*1 “Mke wa mtu mmoja kutoka katika wana wa manabii akamwendea Elisha, akamwambia, “Mtumishi wako mume wangu amekufa, nawe unajua alikuwa anamcha BWANA. Lakini sasa yule anayemdai anakuja kuchukua wanangu wawili kama watumwa wake.”*

*2 Elisha akamjibu, “Nitawezaje kukusaidia? Niambie, una nini ndani ya nyumba yako?” Akasema, “Mtumishi wako hana kitu cho chote kabisa isipokuwa mafuta kidogo.”*

*3 Elisha akasema, “Zunguka kwa majirani zako wote ukaombe vyombo vitupu. Usiombe vichache.*

*4 Kisha ingia ndani na ujifungie mlango wewe na wanao. Mimina mafuta kwenye vyombo vyote, kila kimoja kinapojaa, kiweke kando.”*

*5 Yule mjane akaondoka na kujifungia ndani, yeye na wanawe. Wao wakamletea vyombo naye akaendelea kumimina mafuta.*

*6 Vyombo vyote vilipojaa, akamwambia mwanaye, "Niletee chombo kingine." Lakini mwanaye akajibu, "Hakuna chombo kingine kilichobaki." Basi mafuta yakakoma kutiririka.*

*7 Yule mwanamke akamwendea yule mtu wa Mungu, naye yule mtu wa Mungu akasema, Nenda ukayauze hayo mafuta ulipe madeni yako. Wewe na wanao mnaweza kuishi kwa kile kinachosalia.''*

***Vikapu kulisha mataifa***

**Yohana 6:5-13 inasema,**

*5 "Yesu alipotazama na kuuona ule umati mkubwa wa watu ukimjia, akamwambia Filipo, Tutanunua wapi mikate ili watu hawa wale?"*

*6 Aliuliza swali hili kumpima, kwa maana alishajua la kufanya.*

*7 Filipo akamjibu, "Hata fedha kiasi cha dinari mia mbili**a**, hazitoshi kununua mikate yakuwapa watu hawa kila mtu apate kidogo.''*

*8 Mmoja wa wanafunzi wake, aitwaye Andrea, ndugu yake Simoni Petro, akamwambia,*

*9 "Hapa kuna mvulana mmoja mwenye mikate mitano ya shayiri na samaki wawili wadogo. Lakini hivi vitatosha nini kwa umati wote huu?''*

*10 Yesu akasema, "Waketisheni watu chini.'' Palikuwa na majani mengi katika eneo lile, nao watu wakaketi, palikuwa na wanaume 5,000.*

*11 Ndipo Yesu akachukua ile mikate, akamshukuru Mungu na kuwagawia wale watu waliokuwa wamekaa kwa kiasi walichohitaji. Akafanya vivyo hivyo na wale samaki. Kila mtu akapata kadri alivyotaka.*

*12 Watu wote walipokwisha kula na kushiba, akawaambia wanafunzi wake, "Kusanyeni vipande vilivyobaki vya ile mikate, kisipotee cho chote.''*

*13 Hivyo wakavikusanya wakajaza vikapu kumi na viwili kwa vipande vilivyobaki vya ile mikate mitano na samaki wale wawili wadogo.*

***Kihenge cha kulisha nchi***

**Mwanzo 41:46-49 inasema**

*46 "Yosefu alikuwa na miaka thelathini alipoingia katika utumishi wa Farao mfalme wa Misri. Naye Yosefu akatoka mbele ya Farao akasafiri katika nchi yote ya Misri. akasafiri katika nchi yote ya Misri.*

*47 Katika ile miaka saba ya neema nchi ilizaa mazao kwa wingi sana.*

*48 Yosefu akakusanya chakula chote kilichozalishwa katika ile miaka saba ya neema nchini Misri, akakihifadhi katika ghala za miji. Katika kila mji kulihifadhiwa chakula kilichozalishwa katika mashamba yaliyouzunguka mji huo.*

*49 Yosefu alihifadhinafaka nyingi, mfano wa mchanga wa bahari, ilikuwa nyingi mno kiasi kwamba walishindwa kuweka kumbukumbu kwa sababu akiba ilizidi sana kupita kipimo."*

**Tafakati kuhusu haya maandiko. Paulo alitaka Wafilipi wabarikiwe**

**Wafilipi 4:15-19 inasema,**

*15 "Zaidi ya hayo, ninyi Wafilipi mnajua kwamba siku za kwanza nilipoanza kuhubiri Injili, nilipoondoka Makedonia, hakuna kanisa jingine lililoshiriki nami katika masuala ya kutoa na kupokea isipokuwa ninyi.*

*16 Kwa maana hata nilipokuwa huko Thesalonike, mliniletea msaada kwa ajili ya mahitaji yangu zaidi ya mara moja.*

***17 Si kwamba natafuta sana yale matoleo, bali natafuta sana ile faida itakayozidi sana kwa upande wenu.***

*18 Nimelipwa kikamilfu hata na zaidi, nimetoshelezwa kabisa, sasa kwa kuwa nimepokea kutoka kwa Epafrodito vile vitu mlivyonitumia, sadaka yenye harufu nzuri, dhabihu inayokubalika na ya kumpendeza Mungu.*

*19 Naye Mungu wangu atawajaza ninyi kila mnachohitaji kwa kadiri ya utajiri Wake katika utukufu ndani ya Kristo Yesu."*

John Wesley alisema "Dhamana ya kitu halisi ni gharama itakayo leta milele

**Muhutasari:**

**11. Kiongozi ni lazima adumishe uhusiano wa nguvu naye Mungu.**

Kila Mkristo, hasa kiongozi ni lazima kuendelea amsikie Mungu akinena.Hiyo si rahisi mpaka mmoja afanye mazoezi ya uhusiano na ujuzi na nguvu za Mungu.

**Ujuzi wa uhusiano.**

**a. Fanya hatua muhimu kufuata uhusiano.**Jipatiane kabisa kwake Mungu.Tafakari katika Warumi 12:1-2 Hii ni kukumbarika kwa damu la agano kwa ukuu wa damu ya agano iliyotolewa naye Mungu.

**b. Chukua muda kusukiliza.**Ni lazima ulisome Neno lake .Maneno ni vyombo vya damu la agano.Neno la Mungu ni Yesu mwenyewe, si kitabu ya ahadi za kuchukua na kuchagua.Neno lake Mungu ni lazima lifuatwe mara kwa mara na kwa uhusiano wa kila siku, na inapaswa kuangaliwa na kusikiliza Mungu wako, Yesu mwenyewe, uliza yeye aongee Neno nila kiungu ,na huzaa imani vile tu chakula za kawaida hutupa nguvu.Yesu akasema yeye ni mkate wa kweli, unaopatiana uzima wa milele.Andika vile unahisi yeye ananena.

**c. Chukuwa muda wako,kunena maneno yako.**Ni mwenendo wa kuwili, na kuwa kwa kiwango cha kuaminika ni ya muhimu sana,kuongeza uhusiano wako na Mungu.Andika kabisa unajihisi aje.Aminika na mwenza wako wa agano la damu, Yesu atasababisha dhambi zake zimwendee yeye.Huwezi na hutaweza kushinda jambo lolote maishani mwako bila kiwango cha kuaminika.Tunafikiri njia za kuwili.Hii ni njia kuu ya kuruhusu "mtiririko" wa Roho Mtakatifu kuongea kwako wewe kwa njia ya kipekee naya karibu sana.Kwanza ,jipate kwa eneo lilo nyamaa sana, weka mawazo yako kwake Yesu na uanze kumwabudu yeye.Andika chini nini unataka kwake Yesu.Tena andika ni nini unasikia ndani ya Roho yako.Kwanza kunaweza kuwa na makosa, lakini kupitia imani na kufanya mazoezi atakuwa halisi kwako.

**Njia za kuelewa sauti gani na ya nani unayo isikia.**

- Sauti ya Mungu**:** Tamka kwa dhati, hurekebisha, hupatia mwelekeo.(ukweli).
- Sauti ya shetani: Hufunga kwa mwanguko na uongo na kulaumu.
- Sauti yako mwenyewe,Mwili wetu:kujiondolea lawama, kulaumu wengine mgawo hukana na kuekelea.

**Kuchunguza ili kujua unamsikia Mungu.**

- Je ni neno?
- Inatukuza Yesu?

- Ina jenga ama ina leta imani chini?
- Kuna ushahindi ndani ya Roho yako?
- Inaleta uhuru ama ufungwa?

**Njia zile Mungu hunena nasi:**

- Bibilia: ufunuo kupitia Roho Mtakatifu.
- Mwili wa Kristo: Waaminio, wahubiri, na washauri.Kuwa mwangalifu usiwategemee kabisa.
- Wakati umenyamaa:Sauti ya Roho Mtakatifu (Zaburi 139:23-24, Yohana 1:9)
- Hali zetu na eneo zetu za maishani kila siku (Yeremia 32;8)
- Mwenza anayewajibika: wakati mwingi ni ya muhimu kuamini rafiki Yule atakuwa nawe, kwa ukali wa hali za maisha haya.

**d. Chukua muda kunena:** Neno lake mpizani shetani, na mapepo wake, mara mingi wamepewa kazi kukuja kinyume cha nguvu zinazo husika na Yesu na kushinda.Niwewe tu unaweza zikata.Yesu alitupa uwezo na nguvu na mamlaka kuja kinyume na kunena neno lake kinyume naoMungu akamwambia Yoshua Joshua 1:8 **"**Usiache Kitabu hiki cha Torati kiondoke kinywani mwako, bali yatafakari maneno yake mchana na usiku, ili upate kuwa mwangalifu kufanya kila kitu sawasawa na yote yaliyoandikwa ndani yake. Ndipo utakapoifanikisha njia yako na kisha utasitawi sana."

**Wazo moja yakufanya nii:**

Soma Zaburi,na Mithali kila asubuhi.Tumia ule mtindo wa kalenda kama kwa mwezi wa tatu soma Zaburi 3,33, 63, 93, na 123.Tena Mithali 3 kwa huu Mtindo mwanafunzi atasoma.Tumia ule mtindo wa kalenda kama kwa mwezi wa tatu soma zaburi 3,33, 63, 93, na 123.Tena Mithali 3 kwa huu Mtindo mwanafunzi atasoma Zaburi mzima na Mithali kwa mwezi.Ukitumia huu mtindo utafanya upya wa akili zako, unanenea shetani Neno, na kuruhusu wanafunzi

wanoteswa kujihusisha na mwandishi wa Zaburi kwa hisia.Matwalio inaweza fanywa kwa miezi kwa siku 31, na kwa zaburi 119;

Tena kuwa mwenye hisia za Roho Mtakatifu mwenye atakupa Neno la **vita kwa hiyo hali.**

**e. Kutafakari:** Kutafakari kwa neno ni ya muhimu sana naya dhamana kabisa .Na nukru Joshua 1:8 inayo twambia tuitafakari usiku na mchana (Zaburi1:2-3)

Kutafakari Neno hutoa na kuweka, kufikiri kwako kwa kimwili iliyo pigo kuu.Tena ina ruhusu Neno likaweze kuingia kilindini cha moyo wako.Kutafakari kwa Neno imelinganishwa na ngombe vile ina cheua .Yeye anacheua, na kumeza, na kurudisha mdomoni tena inarudia hivyo hivyo.Hii hufanya neno la Mungu liingie ndani ya moyo wako, na itampa Roho Mtakatifu nafasi ya kuongea kitu cha binafsi kwako kutokana na neno.

**f.Kufunga:** Kufunga ni nidhamu ya muhimu .Kuna kufunga kwa aina nyingi na sitaweza kunena hili somo hapa.Jambo kubwa njema ya kufunga ni kwamba hukataza shauku kuu ya mwili, kukula.Kwa kufanya hivyo mtu anaweza kusikia Roho mtakatifu vyema.Kumbuka , mwili hutamani kinyume na Roho na Roho kinyume na mwili (Wagalatia 5:17)Nimesoma ya kwamba hata wakati mtu ako na njaa kwa husikia vizuri.

**g. Tii Mungu :**uliza Mungu akupe jambo ndogo hiyo siku ndio uweze kutii.Inaweza kuwa nikutia watu wengine moyo , inaweza kuwa ni kupitia njia nyingine inayo kuelekeza kwa majaribu, inaweza kuwa ni kukili dhambi zako kwake .Inaweza kuwa ni kuchukuwa na kuweka fikira zako chini ya utiiifu, amakusamehe mtu ama pengine kupeana pesa.

Hii ni jambo kubwa! Yohana 14:21-23inasema, kwamba wakati tuna tii Neno lake ya kwamba atajionyesha mwenyewe kwetu.Moja tu unapo “mwona”Yesu uhusiano wake nawe hautakuwa nidhamu, Lakini utakuwa jambo la kufuatilia.

**Muhutasari:**

**12. Kiongozi lazima aishi maisha matakatifu.**

Mapema kwa hiki kichitabu nilinena ya kwamba kiongozi ni lazima ajue Kristo ni yeye amefanya awe; ni lazima ajue kijitabulisho chake kama kinacho elezewa na Bwana.Tutakapo jua tu, tuko katika Kristo tunaweza fikiri kuwa ni gani kwa sababu tunajua sisi si wakamilifu tukiwa na huu mwili.Ilhali ikiwa Kristo anaishi maisha yake ndani Yetu na kupitia sisi kawaida tutafanya makosa na dhambi, lakini tunaweza "kuenenda kwa Roho"na kutubu ili tuishi tena.

**Jiangalie kwa kioo – cha Neno**

**Yakobo 1:23-25inasema,**

*23 "Kwa maana kama mtu ni msikiaji tu wa Neno wala hatendi kile linachosema, yeye ni kama mtu ajitazamaye uso wake kwenye kioo*

*24 na baada ya kujiona alivyo, huenda zake na mara husahau jinsi alivyo.*

*25 Lakini yeye anayeangalia kwa bidii katika sheria kamilifu, ile iletayo uhuru, naye akaendelea kufanya hivyo bila kusahau alichosikia, bali akalitenda, atabarikiwa katika kile anachofanya."*

**Mungu anataka uenende ndani ya Roho" Bila hukumu.**

**Warumi 8:1-9 inasema,**

*1 "Kwa hiyo, sasa hakuna hukumu ya adhabu kwa wale walio ndani ya Kristo Yesu, wale ambao hawaenendi kwa kuufuata mwili bali kwa kufuata Roho.*

*2 Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima katika Kristo Yesu imeniweka huru mbali na sheria ya dhambi na mauti.*

*3 Kwa maana kile ambacho sheria haikuwa na uwezo wa kufanya, kwa vile ilivyokuwa dhaifu katika mwili, Mungu kwa kumtuma Mwanawe mwenyewe kwa mfano wa mwanadamu mwenye*

*mwili ulio wa dhambi na kwa ajili ya dhambi, Yeye aliihukumu dhambi katika mwili,*

*4 ili kwamba haki ipatikanayo kwa sheria itimizwe ndani yetu sisi, ambao hatuenendi kwa kuufuata mwili bali kwa kufuataRoho.*

*5 Kwa maana wale wanaoishi kwa kuufuata mwili huziweka nia zao katika vitu vya mwili, lakini wale wanaoishi kwa kufuata Roho,huziweka nia zao katika mambo ya Roho.*

*6 Kwamaana kuwa na nia ya mwili ni mauti, bali kuwa na nia inayoongozwa na Roho ni uzima na amani.*

*7 Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui na Mungu, kwa maana haiitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii.*

*8 Wale wanaotawaliwa namwili, hawawezi kumpendeza Mungu.*

*9 Lakini ninyi, hamtawaliwi na mwili, bali na Roho, ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu. Mtu ye yote ambaye hana Roho wa Kristo, yeye si wa Kristo."*

Kwa urahisi uliza Mungu kuendelea akushindilie, tena ukili dhambi zako na utubu.Na ya muhimu ni kukumbuka kwamba Mungu atakuepusha kutokana na "adui" zako zile zako wanao sambambisha utende dhambi.

**Muhutasari:**

13**. Kiongozi lazima afanye mazoezi kwa kunena kifupi.**

Kunena na wengine ni jambo sisi zote tunastahili kweli kufanyia kazi.Sisi zote si wakamilifu kwa kunena.Mara nyingi hawaelewi ni nini iko ndani yetu, mara nyingi maneno yetu humaanisha jambo lingine halikuwa limekusudiwa.Jambo moja la muhimu na huwa linasahaulika ujuzi ni kusikiliza.Kwa kusikiliza ni

lazima tung'ang'ane "kujiweka ndani ya viatu vya wengine"Hisi vile wanaweza hisi.Kwa njia hiyo ikiwa hutanena kuwili kuliko kuongea tu, na watu wasio jibu.

**Kutatua matatizo.**

Sisi zote tutakambiliana na mapigo kwa njia moja ama nyingine . Kutatua mapigano mara nyingi ni jambo la kutamanika.Wakati mwingi mapigano hayawezi kutatuliwa, nalile tu jambo linafaa lifanywe ni kusau na kusamehe mtenda dhambi . Hata kama wakati mwingi ni lazima tujishughulishe kutatua shinda.Hatufai kuzika mambo tunafaa kukambiliana nayo, na wakati huo kung'ang'ana kukambiliana kama unaongozwa kwa kuelewa na upendo.

Nimeona mapigano katiaka hali za huduma na haikuweza kutatuliwa lakini kuiacha na kuweza kundunga kwa miaka.Sawa nani alidumisha huduma.Wahusika wote, aliyetendewa na aliyetenda wakachagua kutonena kuhusu hilo jambo.Jua ya kwamba mambo inayo wekwa kwa nuru Yesu anaingililia na ukweli na kwa upendo

***Jambo nakuepuka Kuzungusha kuingia kwa ile jambo halisi.***

Watu wengine wanaishi na tabia ya kuzuia maongeo, ile jambo halisi linahitaji kuzungumziwa.Mbali na hiyo katoke na ulize maswali ama hoja iliyo sawa hao hupendelea kuwa na hoja, ama fahamu jambo.Sina ukweli kwa nini hufanya hivyo, pengine, huja kutoka ndani ya kindonda.Kwa mfano ikiwa unataka kuuliza mtu aje kwa nyumba yako, unafaa useme, "ningependa wewe kuja kutembelea mimi. Unaweza kuja ijumaa kwangu? Lakini kuepuka makambiliano na wengine jaribu kusema.jambo hilo kama hivi. "Nikona upweke. Nahitaji mtu kuja kunitembelea.Lakini sijui ni fanye ni nini.Wewe uko na Neno?

Wakati wasiliana na hao walio chini ya uongozi wako, hakikisha wewe ni aina ya wale walio na huruma na mwelekeo na usemi.Kuwa na hisia, huruma na uwajenge.Hakikisha eti wanajua

hao ni wa muhimu. Wajenga katika Bwana wasikilize na uheshimu hisia na mawazo yao hata kama wamekosa! Kwa upole walete kwa ukweli, kuliko kuwagombanisha kwa kuwa na makosa, lakini usiogope kikambiliana nao na “ukweli katika upendo”

Mwishowe kuwa mwangalifu kwa vile unaeleza uongozi.Usi “jifanye wewe’”Kiongozi na wanatamani kukufuata.Ikiwa umewekwa kwa nafasi isiyo ya kujitolea kwa uongozi, kila mmoja atakaye kosa kunyenyekea kwa mamlaka, ni lazima ushughulike kwa hiyo hali na maombi mengi na unyenyekevu.

**Muhutasari:**

**14. Siri ya mwisho**

Tulianza hiki kitabu na siri ya ajabu kwamba Kristo huishi ndani yako,na kwamba ni kiongozi pekee na tunastahili kumruhusu yeye aishi maisha yake kupitia sisi. Sasa, tungependa kuongeza siri kwa hii.

Kama kiongozi na mfuasi wake Yesu Kristo, kabisa utakutana na majaribu, mateso na vita za kiroho. Shetani atatumia wanao imba ndoto kama Marko 4. Shetani huja kuimba mbegu ile Mungu amenena maishani mwako.Wasamehe hao na uendelee.Ilhali kuongeza kwa wanao imba ndoto na kuta kuwa na mateso ile itajaribu kukunyanganya, ndoto na maono. Kumbuka kwamba Mungu si yeye ana leta mateso maishani mwako.(Ayubu sura 1)

**Ni Kiongozi lazima ajue kwamba matunda huongozwa na mateso.**

**Waebrania 2:10 inasema,** *10 “Ili kuwaleta wana wengi katika utukufu, ilimpendeza Mungu, kwa ajili Yake na kwakupitia*

*Yeye kila kitu kilichopo, kumkamilisha mwanzilishi wa wokovu wao kwa njia ya mateso."*

Ikiwa tuna tembea kwa uhusiano wa karibu sana kwa ushirika naye Yesu atatupa amani wakati tunapopitia majaribu. Mara nyingi maishani ataniachia nijue mwenyewe anaelewa ni nini ninayoya pitia na anatembea nami.Hii pekee ni toshereko tosha.

**Siri**

**Wakolosai 1:20**

*20 "na kwa njia ya Mwanawe aweze kuvipatanisha vitu vyote na Yeye mwenyewe, ikiwa ni vitu vilivyoko duniani au vilivyoko mbinguni, kwa kufanya."*

Neno patanisha, linamaanisha kuwa na rafiki kutoka kwa adui, ama kuleta uhusiano wa urafiki kati ya wawili wanao vurugana.Tunajua ya kwamba kama wanadamu, tumeweza kupatanishwa na Kristo.Ilhali hii andiko katika Wakolosai 1:20 inasema ya kwamba Mungu hufanya marafiki kwa kila "kitu.Mateso yetu ni ya mambo.Yeye anafanya nini hiyo?Kupitia damu ya msalaba wake!Muujiza wa msalaba wa Yesu na kumwaga damu, Yule angeweza kukosea binadamu yeyote, kuwa kwa Baraka kuu zile ulimwengu hazina ufahamu wake.

Dhambi, hasa sio yako lakini kwa jumla katika hii dunia, ni chanzo cha uchungu na maumivu. Kwa sababu Yesu alichukuwa dhambi zote, kwa hivyo uchungu na maumivu ya kuja kwako, hukuta hakuna dhambi ya kukudhuru wewe.Kweli, sisi sio wakamilifu, lakini tunaendelea kukili dhambi zetu naye anaendelea kutuweka wa safi. Kwa hivyo, unapoamini haya , uchungu wote, mateso na maumivu ni lazima kwa sheria iwe Baraka.Si wewe unaweza kusema vile ungetaka Baraka ije , kazi yako ni kwamini pekee na kuamini Mungu kwa miujiza mikuu yake ilifanyika kwa kifo na ufufuo wa Yesu.

**Paulo alifurahia kwa mateso yake:**

**Wakolosai 1:24 inasema,**

*24 "Sasa nafurahia kule kuteseka kwangu kwa ajili yenu na katika mwili wangu ninatimiliza yale yaliyopungua katika mateso ya Kristo kwa ajili ya mwili wake, ambao ni Kanisa."*

**2 Wakorintho 12:9-10 inasema,**

*9 "Lakini aliniambia,"Neema yangu inakutosha, kwa kuwa uweza wangu hukamilika katika udhaifu." Kwa hiyo nitajisifu kwa furaha zaidi kuhusu udhaifu wangu, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu.*

*10 Hii ndiyo sababu, kwa ajili ya Kristo, nafurahia udhaifu, katika kutukanwa, katika taabu, katika mateso na katika shida, kwa maana ninapokuwa dhaifu, ndipo nina nguvu."*

Tazama kwamba Paulo hakusema, kwamba alivumilia maumivu na mateso siyo tupu, lakini kabisa alifurahia ndani yake na akawa na raha kwa mateso. Kwa nini alisema haya?

**Paulo alijua siri;**

Tazama katika Wakolosai 1:24 Paulo alisema, kwamba mateso yake ilikuwa inajaza hayo mateso ya Kristo iliyokuwa haipatikani.Paulo akanena kwamba mateso yake ilifanya kazi kwa wema kwa mwili wake Kristo kanisa.Hii inawezekana aje?Nimejifundisha mambo kuhusu hii jambo si tu kwa Roho Mtakatifu, akinena maandiko kwangu, lakini kwa kupitia mimi mwenyewe.

Yesu alilipa deni yote ya dhambi pale msalabani na kwa ufufuo wake akafanya itendeke kwetu sisi.Kwa hayo hakuna kitu kilichokosekana.Naamini kilicho kuwa na kinakosekana ni ile inaitwa kufa kwa moyo na kufufuka.Mateso yetu kwa njia za siri, wakati tumerudiana , huleta wengine katika ujuzi wa kuokolewa na Yesu na katika ufalme wake.

**Tazama agano la kale Yusufu kama mfano.**

Yusufu aliteseka sana, mikononi mwa ndugu zake na mikononi mwa watu walio na mamlaka katika Msiri, alipokuwa

mfungwa.Ilhali, pengine ushuhuda wa Yusufu ulikuwa “lakini Mungu alikuwa naye”Wakati alipofunguliwa kutoka gerezani na akafanywa kuwa waziri mkuu katika Msiri, yeye hakuwa tu amekombolewa na kuzawadiwa, lakini mateso yake ilifanya watu wa Mungu, wana wote wa Israeli waokolewe.Huu ni mfano wa vile mateso yetu itafanya tutakapo vumilia katika imani.

**Tutazame hiki kipengele katika Wakolosai.**

**Wakolosai 1:19-20, 24-27 inasema,**

*19 “Kwa kuwa ilimpendeza Mungu kwamba ukamilifu Wake wote wa kimungu uwe ndani Yake*

*20 na kwa njia ya Mwanawe aweze kuvipatanisha vitu vyote na Yeye mwenyewe, ikiwa ni vitu vilivyoko duniani au vilivyoko mbinguni, kwa kufanya amani kwa damu Yake iliyomwagika msalabani.*

*24 Sasa nafurahia kule kuteseka kwangu kwa ajili yenu na katika mwili wangu ninatimiliza yale yaliyopungua katika mateso ya Kristo kwa ajili ya mwili wake, ambao ni Kanisa.*

*25 Mimi nimekuwa mtumishi wa Kanisa kwa wajibu alionipa Mungu ili kuwaletea ninyi neno la Mungu kwa ukamilifu.*

*26 Siri hii ilikuwa imefichika kwa karne nyingi na vizazi vingi, lakini sasa imefunuliwa kwa watakatifu.*

*27 Kwao, Mungu amechagua kujulisha miongoni mwa watu Mataifa utukufu wa utajiri wa siri hii, ambayo ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu.”*

Tazama matokeo mwishowe, kila Paulo alikuwa naye katika mawazo kupitia mateso yake katika mstari 27.Alijua kwamba mateso yake itaonyesha fumbo nyingi kwamba Kristo Anaishi ndani yao! Nakubali hivi mara mingi njia tu ya pekee , vile Mungu anaweza dhihirisha siri zake kwa wengi ni kupitia mateso yetu.Niko na shuhuda za kipekee kuhusu hii vile amenishangaza!

**Kuweka kwa pamoja. Ina husu kufa na kufufuka kwa nafsi**



## Nafsi Yako = mapenzi, akili, hisia



Wakati tulipokoka tuliweza kupokea Roho ya ufufuo wake Yesu.Wakati tunapoenda mbinguni tutapokea miili yetu iliyofufuka kwa muda nafsi zetu ziko hapa zikiwa na hali ya kuto kamilika.Hii ni hiali yetu , mawazo na hisia zetu.Wakati tunapopitia kwa mateso na uchungu hii ni kifo cha nafsi zetu.Ni kwa haya tunaweza itwa "washindi"Tunapopitia bonde la kivuli cha kifo tukiamini na kuabudu Mungu kwa yote, mioyo yetu huelewa kufufuka kama tunapitia haya maisha.Wakati hii inatendeka nguvu zile zilimshinda shetani kupitia ufufuo wa Kristo kushinda adui kwa eneo letu la utawala,na tunazaa matunda mengi kama vile Kristo alifanya kupitia ufufuo wake! Kuna maandiko mingi ya kudhibitisha haya yote, lakini si jihisi kwamba hii nakala itaturuhusu tuenende kwa mengi ya hii kwa ndani: Hapa kuna mawili.

**Yohana 12:24 inasema,**

24 "Amin, amin, nawaambia, mbegu ya ngano isipoanguka ardhini na kufa, hubakia kama mbegu peke yake. Lakini ikifa huzaa mbegu nyingi."

***Kushinda kunahusu kifo cha mioyo yetu.***

**Ufunuo 12:11 inasema,**

*11" Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo na kwa neno la ushuhuda wao. Wala wao hawakuyapenda maisha yao hata kufa."*

***Huu mtindo kwamba Mungu alipitishia Abrahamu.***

Agano la damu linahitaji vifo mbili damu ya wahusika wawili. Yesu aliweza kuchukuwa msalaba wake na kuruhusu kusulubiwa kwake. Hii ilikuwa sehemu yake.

***Sehemu ya kwanza: Sehemu ya Mungu*:**

**M**ungu alinena ahadi zake kwa Abrahamu katika Mwanzo sura 12.Hiyo ilikuwa ahadi kubwa kwa mtu hakuwa na mtoto.Kwa hali ya uhalisi, Abrahamu na Sarai hawangeweza kupata mtoto.

**Mwanzo 12:2 inasema,**

*2 "Mimi nitakufanya taifa kubwa na nitakubariki, Nitalikuza jina lako, nawe utakuwa baraka."*

Mungu ananena na Abrahamu kuhusu Maono katika Mwanzo sura ya 15.

**Mwanzo 15:5 inasema,**

*5 "Akamtoa nje na kusema, ''Tazama juu kuelekea mbinguni na uhesabu nyota, kama hakika utaweza kuzihesabu.'' Ndipo akamwambia, ''Hivyo ndivyo uzao wako utakavyokuwa.''*

Abrahamu alihitaji uwepo wa Mungu ili aweze kuamini ahadi Zake Mungu. Hivyo basi, Abrahamu akamuomba Mungu amsadiye kuamini.

**Mwanzo 15:8 inasema,**

*8 ''Ee BWANA Mwenyezi, nitawezaje kujua kwamba nitapata kuimiliki?''*

Mungu akajirubi swali hilo kwa sherehe ya agano la damu. Sherehe huelezea kuhusu msalaba na damu itakayo mwagwa na Yesu siku zi jazo.

**Mwanzo 15:9-10 inasema,**

*9 "Ndipo BWANA akamwambia, ''Niletee mtamba wa ng'ombe, mbuzi na kondoo mume, kila mmoja wa miaka mitatu, pamoja na hua na kinda la njiwa.''*

*10 Abramu akamletea hivi vyote, akampasua kila mnyama vipande viwili, akavipanga kila kimoja kuelekea mwenzake, lakini hata hivyo ndege, hakuwapasua vipande viwili."*

Katika msalaba wa Yesu hatukuwa na nafasi, Mungu alimweka Abramu kwa usingizi. Siyo Abramu wala sisi tunazo hurumu za kumwaga damu kwa niaba ya Mungu.

**Mwanzo 15:12 inasema,**

*12 "Wakati jua lilipokuwa linatua, Abramu akashikwa na usingizi mzito, giza nene na la kutisha likaja juu yake."*

Mambo mawili yanayo husika katika mtaro wa agano la damu, kwa mawazo yangu, Mungu alijihidhilisha kwa njia mbili,

tanuru la moshi na mwali wa moto. Tanuru la moshi lina dhihilisha ghadhabu ya Mungu. ghadhabu yote ya Mungu ikawa juu ya Yesu.

**Mwanzo 15:17 inasema,**

*17 "Wakati jua lilipokuwa limeshatua na giza limeingia, tanuru la moshi na mwali wa moto unaowaka vikatokea na kupita kati ya vile vipande vya nyama."*

**Sehemu ya pili: Sehemu ya moja. Nafsi iliyo kufa.**

Kama nimeelezea kwa vitabu vingine, hasa "Grow or Die" sura ya "The flowing River", tunaweza beba msalaba tunapo shika mateka akili zetu, mapenzi na hisia kufanyisha mazoezi mambo ya kiungu, lakini kwa urahisi ni ‘ kuchukua juu." Baadaye, lazima kuwe na kusulubiwa kwa ukweli kwa hisia zetu.

Wakati Yesu alisulubiwa na kufufuka kutoka kifo, alimaliza sehemu yake ya agano la damu.Alitupatia haki ya kuwa wana ufufuo wa Roho Mtakatifu, na kuungana na Roho zetu.Alitupatia haki ya kupata ufufuo wa mwili wakati miili yetu ya duniani takayo kufa.Ilhali kwa muda hapa duniani nafsi "zetu za kale"bado zinaishi.Hiyo ni jambo hawezi kuitawala.Hiyo iko katika ukuu wa hiari zetu kusema ndio au la kwake.Hii tu ndio inakosekana kwa mateso ya Kristo, ni kwa kupenda kwetu tunachukuwa msalaba wetu kuweka nafsi zetu mbele zake Mungu,kama dhambihu iliyokubalika.Kama inavyosema katika Warumi 12:1-2.Wakati tunachukuwa msalaba wetu, inamaanisha ya kwamba tunapenda kuruhusu nafsi zetu kwenda kupitia kiufo na ufufuo.

**Kifo cha nafsi ya Abrahamu.**

**Mwanzo 22:1-2 inasema,**

*1 "Baadaye Mungu akamjaribu Abrahamu. Akamwambia, "Abrahamu!'' Abrahamu akajibu, "Mimi hapa.''*

*2 Kisha Mungu akamwambia, "Umchukue mwanao, mwana wako wa pekee, Isaki umpendaye, uende katika nchi ya Moria. Mtoe huko kama sadaka ya kuteketezwa juu ya mlima mmojwapo nitakaokuambia.''*

Jaribu kuwaza hii. Huwezi ukawa na watoto, Ilhali ahadi zake Mungu ya kwamba hatakuwa tu na watoto lakini watakuwa wengi kama waziwani na nyota wa angaani na itatumika kwa njia kuu ya ukombozi wa mwanadamu.Tena kwa njia isiyo ya kawaida, uko na mtoto, lakini ngoja.Tena Mungu akakunenea umuue mtoto kama dhabihu kwake.Niambie mimi:Unaweza jihisi aje?Nafsi yako inaweza kufa?Lakini bado Abrahamu aliamini Mungu kabisa hakutaka tu kumtii Mungu lakini wazo tu , ya kwamba hata akimuua mwana wake Mungu anaweza mfufua , kutokana na kifo ndio atatimize ahadi zake.

**Waebrania 11:17-19inasema,**

*17 "Kwa imani Abrahamu, alipojaribiwa na Mungu, alimtoa Isaki kuwa dhabihu. Yeyealiyekuwa amezipokea ahadi za Mungu alikuwa tayari kumtoa mwanawe, aliyekuwa mwanawe pekee awe dhabihu.*

*18 Ingawa Mungu alikuwa amemwambia Abrahamu, "Uzao wako utahesabiwa kwa njia ya Isaki,''*

*19 Abrahamu alihesabu kuwa Mungu angaliweza kumfufua Isaki kutoka kwa wafu na kwa kusema kwa mfano alimpata tena Isaki kutoka kwa wafu."*

Vile tu, Abrahamu ali mtii Mungu aliinua dhabihu ya kutolewa, iliyodhihirisha Kristo.

**Mwanzo 22:12-13inasema,**

12 "Akamwambia, "Usimdhuru kijana, wala usimtendee jambo lolote. Sasa ninajua kwamba unamcha Mungu, kwa sababu hukunizuilia mwanao, mwana wako wa pekee.''

13 Abrahamu akainua macho yake, akaona kondoo mume amenaswa pembe zake nyuma yake katika kichaka. Akaenda akamchukua huyo kondoo mume, akamtoa awe sadaka ya kuteketezwa badala ya mwanawe."

**Huo ulikuwa ufunuo wa nafsi ya Abrahamu.**

Baada ya kifo na ufufuo wa nafsi zetu , tumeshikanishwa katika damu ya agano kwa kifo cha ufufuo wa Yesu kwa njia mpya .Sisi tumeshaunganishwa kwa damu ya agano kwa kuzaliwa upya kwetu,kwa sababu huo ndio wakati kifo cha moyo wetu kilichoa fanyika kwanza.Tulikataa kufa kwa kujitegemea kwetu na tufanya Yesu kuwa Bwana .

Ilhali kama sisi tutaenenda kupita kifo cha nafsi tumeunganishwa kwa nguvu za agano la Mungu.Kwa njia kuu sana mbali sana utu wetu wa kuelewa kuzaa matunda mengi

***Tazama vile Mungu alimtuma Abrahamu sasa.Mtumwa wa kipekee akiahidi matunda mengi.***

Mungu alifanya ahadi mwanzoni, lakini sasa Abrahamu aligeuza mateso yake kuwa rafiki mazao, mazao ilipewa hali utakayopitia.

**Mwanzo 22:15-18 inasema,**

*15 "Basi malaika wa BWANA akamwita Abrahamu kutoka mbinguni mara ya pili,*

*16 akasema, "Ninaapa kwa nafsi yangu, asema BWANA, kwamba kwa sababu umefanya hili na hukunizuilia mwanao, mwana wako wa pekee,*

*17 hakika nitakubariki na nitauzidisha uzao wako kama nyota za angani na kama mchanga ulioko pwani. Wazao wako watamiliki miji ya adui zao,*

*18 kupitia uzao wako mataifa yote duniani yatabarikiwa, kwa sababu umenitii.''*

**Ahadi ya ufanisi baada ya kifo cha nafsi yako**

**3 Yohana 1:2inasema,**

2 "Mpenzi, naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako kama vile roho yako ifanikiwavyo."

**Ufalme wa Yesu unafanya kazi kama tunda**.

Tunda, kama zabibu iko na nguvu za kukua. Kila tunda lina mbegu mbili ama nyingi, si tu mbili ni zaidi. kadilia kila zabibu ina

1,000 zabibu, inaweza kuwa ongezeko laaina gani! Zalisho la kwanza laweza kuwa kama zabibu 2,000,000.

**Ufalme wa Yesu unafanya kazi kama chachu.**

Chachu huwa na ongezeko kuu la kushangaza. Chachu iko na chembe ya uhai. Na kila sehemu hujigawanya mara mbili, nazo huendelea kujigawanya mpaka chachu imekua kwa njia ya kushangaza!

**Chachu isiyo ya kiungu:**

Katika Marko sura ya 8, Yesu alikuwa anawanenea wanafunzi wake kwa marekabu kuhusu hofu ya kutokuwa na chakula tosha , ama unaweza sema, kutwaliwa kwa maisha.Waliteta tu mkate mmoja, kwa hiyo safari na wakawa na hofu kama wengi wetu.

**Marko 8:13-21 inasema,**

*14 “Wanafunzi walikuwa wamesahau kuleta mikate ya kutosha. Walikuwa na mkate mmoja tu kwenye mashua.*

*15 Yesu akawaonya: ‘‘Jihadharini na chachu ya Mafarisayo na ya Herode.’’*

*16 Wakaanza kujadiliana wao kwa wao wakasema, ‘‘Anasema hivi kwa kuwa hatukuleta mikate.’’*

*17 Yesu akifahamu majadiliano yao, akawauliza: ‘‘Mbona mnazungumzia kuhusu kutokuwa na mikate? Bado hamtambui wala kuelewa? Je, mbona mioyo yenu ni migumu kiasi hicho?*

*18 Mna macho lakini mnashindwa kuona, mna masikio lakini mnashindwa kusikia? Je, hamkumbuki?*

*19 Nilipoimega ilemikate mitanokuwalisha watu elfu tano, mlikusanya vikapuvingapi vilivyojaa vya masazo?’’ Wakamjibu, “Kumi na viwili.’’*

*20 ‘‘Je ? nilipomega ile mikate saba kuwalisha watu 4,000, mlikusanya vikapu vingapi vilivyojaa vya masazo?’’Wakamjibu, “Saba.’’*

*21 Ndipo akawaambia, Akawauliza, ‘‘Je, bado tu hamwelewi?’’*

**Kwa nini Yesu alionya kuhusu chachu ya Wafalisayo na chachu ya Herodi?**

***Chachu za Wafarisayo***

Chachu za wafarisayo ni utakatifu wa kibnafsi.Hao hugeuza Neno la Mungu toka chini na juu, wa kitazama hali iliyo ya kiwiliwili lakini wanakiuka kanuni na amri zake Mungu Walitarajia ya kwamba kutii kwa kiwiliwili kwa sheria inaweza sababisha ashughulike kwa mahitaji ya muda mfupi;

***Chachu ya Herodi***

Herod anaonyesha "mipango ya kidunia"Herodi anawakilisha "uongo uzinzi',Unyanganyi wa utawala, kuumiza wengine ndio kujiinue wewe mwenyewe.Ni kama shirika la kidunia. Kwa sasa na hata mengi kama watu wengine, wanao endelea kujaribu kuiba ,na kukula na wengine huishi kwa raha za uzizi.Yesu alikuwa akiwaambia wanafunzi wake ya kwamba kutafuta kwanza ufalme wa Mungu, na haki yake na kukungojea chachu ya ufalme , kuleta wingi katika maisha yao. (Mathayo 6: 33)

***Chachu ya kiungu:***

**Mathayo 13:33 inasema,**

*33 "Akawaambia mfano mwingine, ''Ufalme wa Mbinguni unafanana na chachu ambayo mwanamke aliichukua akaichanganya katika vipimo vitatu vya unga mpaka wote ukaumuka*.''

Kile Yesu alikuwa anasema haswa katika kifungu cha 13 cha Mathayo yote ni kwamba, kama tutashikamana na ufalme wake tutaweza kuishi maisha ya kuzaa mazao mengi siyo tu kwa ajili ya maisha yetu lakini pia kwa yake.Kila ambacho ninasema ni kwamba njia pekee ya kupokea uwezo wetu ni kuzaa matunda ya kiroho zaidi

ya vile tunavyo weza kufikiria ni kupatana na Mungu katika kifo na ufufuo wa nafsi zetu kama vile nimekuwa nikielezea.

**Amosi 9:13 inasema,**

*13 "Siku zinakuja,'' asema BWANA, "wakati mvunaji atakapotanguliwa na mkulima na mpanzi atakapotanguliwa na yeye akamuaye zabibu. Divai mpya itadondoka kutoka milimani na kutiririka kutoka vilima vyote."*

Sikujifunza haya tu kwa kulisoma tu Neno ingawa ni kweli iko katika Neno mbali nilijifunza siri hii katika kupokea kifo cha nafsi yangu.Wakati niliona matunda ya kianza kuonekana sikuweza kuongea karibu ni shindwe.Ni jambo la kustajabisha ama la kuingia katika mapumziko ya Mungu ilhali ukitazama matunda ya kiingia katika maisha yako matunda ambayo huwezi kamwelezea , yamepatikana ila tu ni Mungu amefanya kazi.

Je, yawezekana Yule kijana mdogo au wanafunzi katika Yohana sura 6.Kuelezea ama kujidai kuliisha wale watu 5,000 kwa samaki 2 na mikate 5? Hebu fikiria vile yule kijana alimwambia mamake alipofika!Mama afadhali ungemuona Yule mtu alifanya!Jee tunatakikawa kuona tunda hili aje, nina mawazo ya aina gani, yana yoweza leta?

**Yesu akasema kwamba tunaweza pokea uhai teletele.**

**Yohana 10:10 inasema**

*10 "Mwivi huja ili aibe, kuua na kuangamiza. Mimi nimekuja ili wapate uzima kisha wawe nao tele."*

Maana hasa ya jina kuzidishiwa kwa kigiriki ni: *Maana ya Neno teletele"katika giriki ni 4053 Perissov- perissos(per-is-sos)Zaidi, kuzidi kipimo, ama cheo, hitaji, zaidi na juu, zaidi ya ile inayo hitajika, kuongezeka zaidi kupita kiasi kisicho cha kawaida,jambo zaidi, zaida sana kuliko sana.*

Waweza shindwa kwa nini nilichukua nafasi nyingi hivi katika kijitabu hiki cha uongozi kuhusu mateso yanayo elekeza

katika kuzaa matunda.Jibu langu ni hili. Nionyeshe awaye yeyote anayezaa matunda teletele nami nitakuonyesha kikundi cha watu wanaye fuata mtu aliye kiongozi wao.

**Harufu inayo vuta wengine kwa Kristo:**

Kutoka kwa WatchmanNee - “ATable in the wilderness”

“*Nyumba ikajaa harufu ya mafuta yale” (*Yohana 12:3)

*Katika kuvunja kile kibuyu cha mafuta kwa sababu ya Bwana, ile nyumba .Kule Bethania ikajawa nayale manukato. Kitu kikaachiliwa na wote wakakifurahia na hakuna hata moja angekosa kukipata, jee maana ya hii ni nini? Je ushawahi kutana na mmoja ambaye ameumia sana na yale amepitia yamesababisha akapata kutoshereka ndani ya Bwana pekee yake? Kisha ukapata kuelewa jambo. Hisia zako za kiroho hapo hapo, zitapata kunukia kitu –kizuri – kile Paulo anataja manukato mazuri ya Kristo”Kitu kimeweza kuvunjika katika maisha yale, ili kuachiliakile kilicho ndani ya Mungu mwenyewe na kamwe huwezi kukosa kukitambua.Ndio yale manukato yaliyo jaa ile nyumba kule Bethania bado hujaa kanisa hata leo.Manukato ya Maria kamwe* hayapiti.

**Muhutasari:**